



Chanjo za COVID-19 – Unachohitaji Kujua

- Chanjo inaweza kuwalinda watu dhidi ya kupata COVID-19. Ikiwa watu wataambukizwa, pia inawalinda dhidi ya kuwa wagonjwa sana kutokana na COVID-19.
- Pfizer ni chanjo ya mRNA. Huwezi kupata COVID-19 kutoka kwa chanjo hii.
- Watoto na vijana walio na umri wa miaka 5 na zaidi watahitaji vipimo viwili vya chanjo ya watoto ya Pfizer ili kuchanjwa kikamilifu. Huwa umechanjwa kikamilifu siku 14 baada ya kipimo chako cha pili.
- Ikiwa mtoto wako ana umri wa kati ya miaka 5 na 11 na atapokea vipimo vyote viwili kabla ya kufikisha umri wa miaka 12, atapokea vipimo viwili vya chanjo ya watoto. Kipimo chake cha kwanza na cha pili kitakuwa na nafasi ya angalau wiki 8.
- Ikiwa mtoto wako atapokea kipimo cha kwanza akiwa na umri wa miaka 11, atapokea chanjo ya watoto kwa kipimo cha kwanza. Ikiwa atafikisha umri wa miaka 12 kufikia wakati wa kipimo chake cha pili, atapokea chanjo ya vijana/watu wazima kwa kipimo cha pili. Kutakuwa na kipindi cha angalau wiki 8 kati ya vipimo.
- Ikiwa mtoto wako ana umri wa miaka 12 au zaidi, atapokea vipimo viwili vya vijana/watu wazima baada ya kipindi cha angalau siku 28 kati ya vipimo. Hata hivyo, inapendekezwa usubiri kwa wiki 8 kati ya vipimo.
- Virusi vya COVID-19 hubadilika. Hivi huitwa vibadala. Vibadala vingine, kama kibadala cha Delta, huenea upesi zaidi na vinaweza kufanya watu wazima wenye umri mdogo, watoto na vijana kuwa wagonjwa zaidi. Chanjo za COVID-19 hutoa ulinzi dhidi ya vibadala.
- Maelezo zaidi ya kumsaidia mtoto wako kuchanjwa yanapatikana katika <https://novascotia.ca/coronavirus/vaccinate-ns/>



Kupata Chanjo ya COVID-19

- Chanjo ya COVID-19 ni ya bila malipo. Kila mtu aliye na umri wa miaka 5 na zaidi ndani ya Nova Scotia anaweza kupata chanjo ikiwa anaitaka.
- Mtoto wako atahitaji vipimo viwili ili kuchukuliwa kuwa amechanjwa kikamilifu. Huwa umechanjwa kikamilifu siku 14 baada ya kipimo chako cha pili.
- Unahimizwa kwa dhati kupanga miadi kwa ajili ya mtoto wako mtandaoni kwenye novascotia.ca/vaccination
 - Utahitaji kadi ya afya ya Nova Scotia na anwani ya barua pepe au nambari ya simu ili kuweka nafasi mtandaoni
- Ikiwa huwezi kuweka nafasi mtandaoni, unaweza kupanga miadi kwa ajili ya mtoto wako kupitia kwa simu. Piga simu kwa **1-833-797-7772** (bila ada)
 - Huhitaji kadi ya afya ili kuweka nafasi kupitia kwa simu
 - Unaweza kuomba kupata mkalimani ukipiga simu kwa nambari hii
- Watoto na vijana, kama watu wazima, wanaweza kupata athari ndogo kama maumivu ya misuli, kuhisi uchovu, joto kiasi au uchungu kwenye mkono mahali ambapo sindano ya chanjo ilichomwa. Hii ni kawaida. Inamaanisha kwamba chanjo inafanya kazi na inafunza mwili wao jinsi ya kupambana na virusi.



Kuwa sehemu ya suluhisho letu.

NOVA SCOTIA